

Maswali

1. Daudi alitaka kuleta nini Yerusalemu?
2. Sanduku la Mungu lilijukuliwa namna gani mara ya kwanza?
3. Nini ilifanyikia sakafuni penye wanapuria nafaka?
4. Nini ilifanyika kwa Uza?
5. Daudi alitengeneza nini Yerusalemu?
6. Daudi alikumbuka nini juu ya amri za Mungu kuhusu kulibeba Sanduku?
7. Mara ya pili Daudi alileta Sanduku Yerusalemu namna gani?
8. Daudi alitaka kujengea Sanduku la Mungu nini?
9. Mbona Mungu alisema Daudi hawezi kumjengea Hekalu?
10. Mungu aliahidi Daudi nini? (Ahadi 5)

Majibu

1. Daudi alitaka kuleta Sanduku la Mungu Yerusalemu.
2. Sanduku lilibebwa kwa gari mpya likivutwa kwa ng'ombe.
3. Njia haikuwa laini. Ng'ombe walijikwaa. Uza alishika gari.
4. Mungu alipiga Uza na akafa pale kando ya Sanduku.
5. Daudi aliundia Mungu hema (Maskani) isio ya kawaida.
6. Sanduku lazima libebwe na makuhani kwa miti mbili iliyopita ndani ya pete.
7. Daudi alitii amri za Mungu kikamilifu. Walifurahi na kuimba.
8. Daudi alitaka kujengea Sanduku la Mungu Hekalu ya ajabu.
9. Daudi hangejengea Mungu Hekalu kwa sababu alikuwa ni mtu wa vita.
10. Daudi atakuwa mashuhuri; wazao wa Daudi watakuwa wafalme; mwana wa Daudi atajenga Hekalu; mzao wa Daudi asiye wa kawaida atakuwa mwana wa Mungu. Atatawalia Yerusalemu katika kiti cha Daudi milele.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 2 Mwaka wa 2

64 Daudi anakuwa Mfalme

Kwa Biblia

2 Samweli milango ya 6 na 7

Kiini cha somo

Kuonyesha upendo wa Daudi kwa Mungu. Alitaka Mungu awe katika maisha yake. Mungu aliahidi Daudi mambo makuu

Somo

Baada ya kifo cha Sauli, Daudi alikuwa Mfalme wa Israeli. Daudi alikuwa Mfalme mzuri. Daudi alifanya Yerusalemu kuwa mji mkuu. Daudi alimpenda Mungu na kumtii. Alipenda Mungu awe katika maisha yake wakati wote. Alifunza watu wake wampende na kutii Mungu.


Miaka mingi kabla ya haya yote, Wafilisti walikuwa wamechukua Sanduku la Mungu halafu wakairudisha Israeli tena. Na hilo Sanduku liliwekwa kwa nyumba ya Abinadabu. Lilikuwa bado kule. Sauli alipokuwa Mfalme, watu walikuwa wamesahau Sanduku la Mungu. Walisahau kuabudu Mungu.

Daudi alitaka Mungu awe katika maisha yake wakati wote. Alitaka alete Sanduku la Mungu Yerusalemu, mji wake mkuu. Daudi alitaka watu wake wakuje Yerusalemu kuabudu Mungu. Daudi alichagua watu 30,000 kutoka kwa Waisraeli. Daudi alienda nao kuleta Sanduku la Mungu Yerusalemu.

Sanduku la Mungu lilikuwa takatifu. Utukufu wa Mungu ulikaa katikati ya makerubi iliyokuwa juu ya Sanduku. Wakati wa Musa, Mungu alikuwa ameamrisha kwamba mtu yeyote asikubaliwe kugusa Sanduku la Mungu. Mtu akigusa Sanduku atakufa.

Mungu alisema lazima Sanduku libebwe kwa miti miwili. Hizi miti zilipita ndani ya pete kwa kila upande wa Sanduku. Makuhani tu ndiyo walikubaliwa kubeba Sanduku. Wakati wa Sauli watu hawakuabudu Mungu vizuri. Walikuwa wamesahau amri za Mungu nyingi. Walikuwa wamesahau amri ya kubeba Sanduku la Mungu.

Daudi alienda kuleta Sanduku la Mungu. Sanduku liliwekwa kwa gari mpya. Hilo gari lilivutwa na ng'ombe. Watu wawili Uza na Ahio walitawazwa kuliongoza. Ahio alitembelea mbele ya gari. Daudi na watu 30,000 pamoja na umati wa watu waliimba na kufurahi kwa sababu Sanduku la Mungu lilikuwa linakuja Yerusalemu. Daudi na watu waliimba wakisifu Mungu na vyombo vya muziki.



Sanduku la Mungu lilifika kwa sakafu ya kupuria nafaka. Njia haikuwa laini. Ng'ombe waliokuwa wakivuruta gari walijikwaa. Uza alinyosha mkono kushikilia Sanduku la Mungu lisianguke. Mungu alikasirika kwa sababu Uza aligusa Sanduku. Mungu alimpiga Uza akaanguka na kukufia pale kando ya hilo Sanduku. Hapo Daudi aliogopa kuendelea na Sanduku.

Daudi alipeleka lile Sanduku kwa nyumba iliyokuwa karibu na pale. Hiyo nyumba ilikuwa ya Obed-Edomu. Hilo Sanduku la Mungu lilikaa kwa nyumba ya Obed-Edomu kwa miezi mitatu. Mungu alibariki nyumba ya Obed-Edomu kwa huo muda wote Sanduku lilikuwa kwake.

Daudi alirudi Yerusalemu. Alitengeneza hema au maskani kubwa ya kuweka Sanduku la Mungu. Halafu Daudi akakumbuka amri ya Mungu vile Sanduku linasitahili kubebwa. Daudi akajua sababu iliyomkasirisha Mungu. Hakuwa ametii amri ya Mungu ya kubeba Sanduku. Alikuwa amesahau kwamba Sanduku la Mungu ni takatifu. Hapo ndio Mungu aliishi.

Daudi alisikia kwamba Mungu alikuwa amembariki Obed-Edomu kwa sababu Sanduku lilikuwa kwa nyumba yake. Daudi akajua kwamba Mungu hakuwa na hasira tena. Daudi alifurahi sana. Alienda kuleta Sanduku la Mungu Yerusalemu.

Daudi alihakikisha kwamba kila kitu kitafanyika vile Mungu aliamrisha. Makuhani waliweka miti mbili ndani ya pete ya Sanduku. Makuhani walibeba Sanduku la Mungu na kulitoa kwa nyumba ya Obed-Edomu.

Daudi alikuwa amechagua nyimbo za maana kuimba na kumsifu Mungu. Sadaka zilitolewa za kumshukuru. Daudi alichezea Mungu kwa furaha. Daudi na kila mtu wa Israeli walileta Sanduku la Mungu Yerusalemu. Kulikuwa na furaha kuu. Makuhani walipiga tarumbeta. Daudi na watu wote waliimba na kucheza wakimsifu Mungu. Wakati Daudi alikuwa Mfalme, watu walikuja Yerusalemu wakiabudu Mungu.

Daudi alikaa kwa jumba nzuri ya Mfalme. Sanduku la Mungu lilikaa kwa hema yenye Daudi alitengeneza. Daudi aliona si vyema yeye kukaa kwa nyumba ya Mfalme hali Sanduku la Mungu liko kwa hema. Daudi alitaka ajenge Hekalu kubwa yenye watu wote wangukuja na kuabudu Mungu. Mungu alimwambia Daudi kwamba yeye ni mtu wa vita. Hawezi kujengea Mungu Hekalu. Daudi aliandaa mawe, mbao, dhahabu na fedha zitakazotumiwa kujengea Hekalu. Solomoni mwana wa Daudi ndiye alijenga Hekalu.

Mungu alifurahi sana kwa sababu Daudi alimpenda na alitaka kumjengea Hekalu. Mungu alimbariki Daudi na akamuahidi ahadi za ajabu.

- ◆ *Daudi atakuwa mashuhuri, mmoja wa watu wakuu ulimwenguni kote.*
- ◆ *Wazao wa Daudi watakuwa wafalme juu ya watu wa Mungu, Israeli*
- ◆ *Daudi atakuwa na mwana atakajenga Hekalu Yerusalemu*
- ◆ *Daudi atakuwa na mzao wa kipekee, na atakuwa mwana wa Mungu*
- ◆ *Huyu mzao wa kipekee atatawala kutoka kwa kiti cha enzi cha Daudi huko Yerusalemu na Ufalme wake ni wa milele.*

Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Yesu atakaporudi hapa duniani, atasimamisha Ufalme wa Mungu Yesu atatawala ulimwengu wote kutoka Yerusalemu kwa kiti cha enzi cha Daudi. Mungu aliahidi Daudi kwamba ataishi milele kwa huo Ufalme hapa ulimwenguni.

Daudi alifurahia sana hizo ahadi zenye Mungu alimwambia. Daudi alikuwa Mfalme mzuri sana. Alitawala Israeli kwa miaka arobaini.